

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE

12 MEI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE – TAREHE 12 MEI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA AFYA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**302. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON
MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali itahakikisha Watanzania wanaofanya kazi kwenye Kampuni za Kichina wanalipwa vizuri kwa mujibu wa Sheria.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**303. MHESHIMIWA NEEMA GERALD
MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanza kutoa Posho kwa Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

**304. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA
(NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa Fedha za ujenzi wa Vituo vya Afya katika Kata za Mnongodi na Nyundo.

305. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo la upungufu wa Walimu wa Sayansi Mkoani Mara.

306. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA (MBARALI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kuboresha Kituo cha Afya Igurusi ili upasuaji uweze kufanyika katika Kituo hicho.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

307. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, lini Serikali itajenga upya na kufanyia ukarabati nyumba zilizo katika Makambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**308. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM
BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Simbo - Kalya yenye urefu wa Km 234.

**309. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Daraja la Lyusa na Itembe na kalavati la Nkoma, Lyusa na Mwanjolo vitajengwa ili Daraja la Sibiti lipitike mwaka mzima.

WIZARA YA NISHATI:

**310. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE
RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Mradi wa Bwawa la kufua umeme RUSUMO utazinduliwa ili kuondoa tatizo la kukatika kwa umeme Ngara.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

311. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itatatia changamoto za mawasiliano ya simu Kata za Milepa, Zimba, Kaengesa na Lusaka.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

312. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kuna mkakati gani wa kukomesha vitendo vya ukatili kwa Wanawake na Watoto.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

**313. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA
(SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi,
Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itaweka alama za mipaka
kutenganisha maeneo ya Hifadhi na Vijiji 975
vilivyotolewa kwenye Hifadhi.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**314. MHESHIMIWA NORA WAZIRI MZERU (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na
Utalii:-

Je, lini Serikali itaweka miundombinu katika
Kivutio cha Utalii cha *Mount Uluguru Waterfalls*.

WIZARA YA KILIMO:

**315. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE
(KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza kugawa maeneo ya kilimo kwa njia ya mnada katika Bonde la Mto Rufiji.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**316. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha VETA Wilaya
ya Kilolo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA AFYA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya
kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA
12 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**